DIRA YA INSHA

MASWALI NA MAJIBU YA INSHA (102/3)

INSHA ZA KIUAMILIFU, MJADALA, METHALI NA MDOKEZO

NA

MWALIMU ONYANGO, DIRA SERIES

MHARIRI: MWALIMU LUCAS ODUOR, UGENYA.

TOLEO LA KWANZA, 2021

TABARUKU KWA WATAHINIWA NA WALIMU WA KISWAHILI

MWALIMU ONYANGO. DIRA SERIES #10. 0707311302. DIRA YA INSHA. HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA. ©2021

SEHEMU YA A: MAAGIZO

MAAGIZO YA 102/1

1. Andika insha mbili Insha ya kwanza ni ya lazima.
2. Kisha chagua insha moja nyingine kutoka hizo tatu zilizobakia.
3. Kila insha isipungue maneno 400

Kila insha ina alama 20

SEHEMU YA B: MITIHANI 30 YA INSHA(KWA NAKALA YA MAJIBU, TUMA 98 KWA 0707311302)

MTIHANI WA KWANZA

1. **Lazima.**
   Wewe umehitmu shahada ya uzamifu kutoka Chuo Kikuu cha Malishoni. Umetuma barua ya kuomba kazi katika taasisi moja inayoshughulika na uhifadhi wa mazingira. Andika tawasifu utakayoiwasilisha kwa wanajopo.

2. Fafanua umuhimu wa viranja shuleni .

3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo: Uzuri wa mkakasi ndani kipande cha mti .

4. Andika insha itakayoanza kwa maneno:

   Siku hiyo nilitoka nyumbani nikiwa nimezongwa na mawazo mengi baada ya mkasa huo.

MWALIMU ONYANGO. DIRA SERIES #10. 0707311302. DIRA YA INSHA. HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA. ©2021

MTIHANI WA PILI

1. Wewe ni kiranja katika shule yako. Andika mahojiano kati yako na mwandishi wa habari kuhusu chanzo cha kuzorota kwa nidhamu katika shule hiyo.
2. Maendeleo ya mwanadamu ndiyo maangamizi yake. Jadili.
3. Andika kisa kitakachodhibitisha ukweli wa methali: usiache mbachao kwa msala upitao.
4. Anza kwa: Nilipowakumbuka wenzangu, macho yaliingia kiwi, machozi yakanilengalenga….

MTIHANI WA TATU

1. Kamati ya uajiri ya kaunti yako imekualika kwa mahojiano ya afisa msimamizi wa kukabiliana na janga la mafuriko. Andika tawasifu utakayoiwasilisha kwa kamati hiyo.

2. Ufisadi umekuwa tatizo sugu nchini. Jadili vyano vyake na upendekeze suluhu kwa uovu huo.
3. Pang'okapo jino pana pengo
   Kisha kidhihirishe maana ifuatayo.

4. Andika insha itakayoanza kwa maneno haya;
   Nilishusha pumzi, nikashukuru. . Masaibu yangu yalikuwa yamefika kikomo na maisha ya siku zijazo yalijaa matumaini.

MWALIMU ONYANGO. DIRA SERIES #10. 0707311302. DIRA YA INSHA. HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA. ©2021

MTIHANI WA NNE

1. Afya yako imezorota. Andika barua kwa mwajiri wako ukiomba likizo ndefu ili upate kukaguliwa na madaktari vizuri.

2. Kutegemea misaada kutoka nchi za ng'ambo kumeletea mataifa machanga madhara.Jadili.

3. Ada ya mja hunena,mwungwana ni kitendo.

4.Andika itakayoanza kwa :Asubuhi hiyo nilishangaa mwalimu mkuu aliponiita na kuniamuru nifunganye…

MTIHANI WA TANO

1. Wewe ni mtangazaji wa kituo cha utangazaji cha Uzalendo. Studioni umetembelewa na mwanamke mtetezi wa haki za wanawake kuzungumzia namna mwanamke ametelekezwa katika jamii ya sasa. Andika mahojiano kuhusu mchakato huo. (Alama 20)
2. Kuna njia anuai zinazoweza kutumiwa kulitandarukia tatizo la ajira nchini. Tetea. (Alama 20)
3. Andika kisa kinachoafiki methali**; Mgagaa na upwa hali wali mkavu.**
   (Alama 20)
4. Tunga kisa kitakacho kamilika kwa kauli ifuatayo;
   …niliduwaa, nikasimama kisha nikaangalia nyuma huku machozi yakinitoka. Nilikumbuka wosia wa walimu na wazazi wangu, lakini kitumbua changu kilikuwa kimeingia mchanga
   (Alama 20)

MWALIMU ONYANGO. DIRA SERIES #10. 0707311302. DIRA YA INSHA. HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA. ©2021

MTIHANI WA SITA

1. Andika barua kwa mhariri wa gazeti la Zindukeni ukitoa maoni kuhusu sekta ya usafiri wa pikipiki.
2. Fafanua njia mbalimbali za kustawisha michezo nchini.
3. Andika insha inayoafikia methali, Ukiona vyaelea vimeundwa.
4. Tunga kisa kinachoanza kwa maneno yafuatayo:

   Nilijaribu kuuinua mguu wangu uliojaa maumivu kutokana na jeraha…..

MTIHANI WA SABA

1. **LAZIMA**

Andika wasifu wa babu yako aliyekuwa mwalimu mkuu katika shule ya upili ya
Tuzo .

2. Wewe ni mbunge wa eneo la Lalama. Pendekeza katika bunge la kitaifa hatua zinazoweza kuchukuliwa na serikali kuu kumwendeleza kielimu mtoto mvulana.

3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo:
   Asiyejua faida ya mwangaza aingie gizani.
4. Tunga kisa kinachoanza kwa maneno yafuatayo:
   Nilipomwangalia baba yangu kisha mama yangu, nilijua kuwa jambo fulani lingetendeka.....

MWALIMU ONYANGO. DIRA SERIES #10. 0707311302. DIRA YA INSHA. HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA. ©2021

MTIHANI WA NANE

1. **Lazima**

   Wewe ni miongoni mwa wanahabari wanaomhoji Inspekta Jenerali wa Polisi katika ofisi yake. Andika mahojiano yenu juu ya hatua ambazo zimechukuliwa kuimarisha viwango vya usalama nchini.

2. Jadili umuhimu wa michezo kwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Kenya.

3. Andika insha itakayothibitisha ukweli wa methali hii.

   Mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani.

4. Andika kisa kitakachomalizikia kwa maneno haya: ... ilinichukua muda mrefu mno kuyaamini yaliyonifika.

MTIHANI WA TISA

1. Wewe kama Mhariri wa Gazet la Ukweli;Ufisadi umekithiri katika taifa la Kenya. Andika tahariri ukieleza chanzo na athari za ufisadi katika uchumi wa Taifa

2. Kutokana na ongezeko la visa vya ukosefu wa usalama,Eleza namna usalama unavyo weza kuimarishwa nchini.
3. Andika kisa kitakachodhibitisha maana ya methali
   Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki
4. Tunga kisa kitakachokamilika kwa maneno haya;
   ……Baada ya hayo yote,alinikumbatia kwa huzuni huku akinishukuru kwa kujaribu kuiokoa hali.

MWALIMU ONYANGO. DIRA SERIES #10. 0707311302. DIRA YA INSHA. HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA. ©2021

MTIHANI WA KUMI

1. Lazima

   Visa vya utumizi wa afyuni miongoni mwa wanafunzi katika taasisi za masomo ulimwenguni vinazidi kuongezeka. Wewe kama afisa mkuu mtendaji katika Tume ya kupambana na Mihadarati nchini umealikwa kuhutubu katika kongamano la Kimataifa lililoandaliwa kujadili suala hili. Andika hotuba.
2. ‘ Haki za mtoto kupata kisomo cha kimsingi zinakiukwa sana nchini’. Fafanua
3. Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali: Jifya moja haliinjiki chungu.
4. Tunga kisa kitakachomalizika kwa maneno yafuatayo;

   …Nilishawishika kuuchukua mtazamo wa pili wa maisha.

MTIHANI WA KUMI NA MOJA

1. **Lazima**

Wewe ni Mwalimu Mkuu katika Shule ya Upili ya Poromoka ambapo pamekuwa na visa vingi vya utovu wa maadili miongoni mwa wanafunzi. Waandikie wanafunzi wote memo ukiwaonya dhidi ya mambo haya.

2. “Utandaridhi una athari mbaya katika maisha yetu.” Jadili.
3. Andika kisa kitakachoafikiana na methali: Bahati ya mwenzio usiilalie mlango wazi.
4. Andika kisa kitakachomalizikia kwa: ... walijifunga vibwebwe kuwavua wahasiriwa waliokuwa wamefunikwa na vifusi lakini jitihada zao ziliambulia patupu.

MWALIMU ONYANGO. DIRA SERIES #10. 0707311302. DIRA YA INSHA. HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA. ©2021

MTIHANI WA KUMI NA MBILI

1. Andika barua kwa mwenyekiti wa Tume ya kupambana na ufisadi ikipitia kwa katibu wa tume hio, huku ukieleza madhara ya ufisadi na jinsi ya kukabiliana na ufisadi nchini. (alama 20)
2. Kugatuliwa kwa huduma za matibabu kutoka serikali kuu kumeleta maumivu kuliko tiba kwa wananchi. Jadili (alama 20)
3. Andika kisa kinachothibitisha ukweli wa methali. (alama 20)
   Pang'okapo jino pana pengo.
4. Tunga kisa kinachomalizia kwa maneno yafuatayo: (alama 20)
   ……kwakweli, penye nia hapakosi njia.

MTIHANI WA KUMI NA TATU

1. Wewe ni mwanahabari wa gazeti la Tomoko Leo. Umemtembelea Mkuu wa Idara ya kupambana na ufisadi Bwana Ridhaa ili kumhoji kuhusu sababu za watu kushiriki ufisadi na suluhisho.

Andika mahojiano yenu.

2. Andika insha kuhusu mambo yanayoathiri utaifa au umoja na utangamano katika nchi ya Kenya.

3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo.

Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe.

4. Tunga kisa kitakachomalizika kwa maneno yafuatayo:

…….Nilipiga darubini kuhusu mawaidha niliyopewa ya mama yangu. Machozi yalinitiririka njia mbilimbili. Utabiri wa mama ulikuwa umetimu.

MWALIMU ONYANGO. DIRA SERIES #10. 0707311302. DIRA YA INSHA. HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA. ©2021

MTIHANI WA KUMI NA NNE

1. **Lazima**.
   Baada ya kumaliza masomo yako ya chuo kikuu, umepata kuteuliwa kushindania tuzo la 'Mwandishi Bora' Afrika Mashariki. Andika tawasifu utakayowasomea mashabiki wako siku hiyo. (Alama 20)
2. Ugatuzi umerahisisha huduma kwa wananchi. Jadili. (Alama 20)
3. Mchuma janga hula na wa kwao. Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali hii. (Alama 20)
4. Andika insha itakayomalizika kwa:
   … Niliyakumbuka maneno aliyosema baba miaka sita iliyopita. Uchungu mwingi ulinitona moyoni na kuyafanya machozi yanidondoke pukupuku. Laiti ningalijua! (Alama 20).

MTIHANI WA KUMI NA TANO

1. Baada ya uchaguzi wa mwaka 2017, suala la Amani na mshikamano wa kitaifa limepewa kipaumbele nchini Kenya. Wewe kama mwanahabari imepata fursa ya kumhoji waziri wa usalama wa ndani kuhusu suala hili. Andika mahojiano mazuri.
2. Asasi ya ndoa inakumbana na changamoto nyingi hapa nchini. Thibitisha kauli hii kwa kurejelea matukio mwafaka.
3. Tunga kisa kinachodhihirisha maana ya methali ifuatayo: Mgema akisifiwa tembo hulitia maji.
4. Andika kisa kitakachomalizika kwa kifungu kifuatacho.
   …Huo ndio mzaha. Mzaha uliokuwa umetibua usaha na kututia katika mashaka haya yote

MWALIMU ONYANGO. DIRA SERIES #10. 0707311302. DIRA YA INSHA. HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA. ©2021

MTIHANI WA KUMI NA SITA

1. Suala la ufisadi limekuwa tatizo sugu katika jamii ya Kenya. Andika hotuba utakayotoa kama afisa wa Tume ya kupambana na ufisadi nchini Kenya kuhusu mbinu za kupambana na ufisadi kwa wanakijiji chenu.

2. Serikali za ugatuzi zitaboresha maisha ya wananchi. Jadili

3. Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.

4. Andika insha itakayoanza kwa maneno yafuatayo: Nilipowakumbuka wenzangu macho yaliingia kiwi na nikaanza kutiririkwa na machozi…

MTIHANI WA KUMI NA SABA

Wewe ni mkaazi wa eneo ya Tushirikiane na unataka kuwania Ugavana katika Kaunti ya Mavuno.

Andika tawasifu utakayowasilisha kwa raia ili waweze kukuchagua.

2.Utandawazi una athari mbaya katika maisha ya vijana. Jadili.

3.Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali: Mwenye kovu usidhani kapoa.

4. Andika kisa kitakachoanza kwa;

Nilikaa pale kwa mseto wa hisia, nisijue kama nilifurahishwa ama nilihuzunishwa na kisa hicho.....

MWALIMU ONYANGO. DIRA SERIES #10. 0707311302. DIRA YA INSHA. HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA. ©2021

MTIHANI WA KUMI NA NANE

1. Wewe ukiwa mwenyekiti wa chama cha msalaba mwekundu shuleni mwako, umemtembelea afisa mshirikishi wa usambazaji msaada wa chakula katika gatuzi lako. Andika mahojiano baina yenu kuhusu changamoto zinazokumba usambazaji huo.
2. Pendekeza hatua zinazofaa kuchukuliwa ili kuimarisha utalii kama kitega uchumi nchini.
3. Andika kisa kinachoafiki ukweli wa methali hii: Achanikaye kwenye mpini hafi njaa.
4. Andika insha itakayoanza kwa:

   "Nilipotazama gazeti la "Tangaza leo," anwani ilinikodolea macho: Shule nyingi zakoza matokeo ya mtihani wa kitaifa KCSE.

MTIHANI WA KUMI NA TISA

1. LAZIMA

   Wewe ni mhariri mkuu wa Gazeti la Mwangaza, andika tahariri kuhusu jinsi ya kuimarisha michezo shuleni hapa nchini.

2. Kunyesha kwa mvua kuna manufaa mengi kuliko hasara. Jadili.
3. Andika insha itakayodhibitisha ukweli wa methali: Mtegemea cha nduguye hufa maskini.
4. Andika kisa kitakachomalizikia kwa maneno yafuatayo … nilimkimbilia mamangu huku machozi yakinibubujika njia mbilimbili, nikashukuru kwa kufika nyumbani salama.

MWALIMU ONYANGO. DIRA SERIES #10. 0707311302. DIRA YA INSHA. HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA. ©2021

MTIHANI WA ISHIRINI

1. **Lazima:**

   Hivi karibuni kumekuwa na visa vingi vya uhalifu hapa nchini vinavyosabishwa na magaidi. Waziri wa usalama nchini ameteua jopo la watu watano watakaochunguza chanzo cha hali hii na kutoa mapendekezo baada ya mwezi mmoja. Andika ripoti utakayowasilisha kwa waziri.

2. Usawa wa kijinsia katika ugawaji wa nafasi za kazi umekabiliwa na vikwazo kadha. Thibitisha.

3. Ukupigao ndio ukufunzao. Thibitisha ukweli wa msemo huu.

4. Andika insha itakayomalizika kwa: …nilipotanabahi nilijikuta mvunguni mwa kitanda.

MTIHANI WA ISHIRINI NA MOJA

1. Wewe ni balozi mteule wa nchi yako katika nchi ya kigeni. Andika tawasifu utakayotoa katika siku ya kutoa stakabadhi zako kwa rais wa nchi uliyoteuliwa kuwa balozi.

2. Utumizi wa afyuni[mihadarati} katika taasisi za masomo nchini ni suala ambalo ni muhali kutatuliwa. Jadili.

3. Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali: Mwenye kovu usidhani kapoa.

MWALIMU ONYANGO. DIRA SERIES #10. 0707311302. DIRA YA INSHA. HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA. ©2021

4. Andika kisa kitakachomalizikia kwa: ... hivyo ndivyo ukurasa mpya katika kitabu cha maisha yangu ulivyofunguka.

MTIHANI WA ISHIRINI NA MBILI

1. Tatizo la udanganyifu katika mtihani wa kitaifa limekithiri nchini. Kama katibu wa jopo lililoteuliwa kuchunguza kiini cha udanganyifu huu, andaa ripoti yako.

2. Andika kisa kitakachoafiki methali;

"Mti mkuu ukingwa wana wa ndege huyumba."

3. Eleza jinsi ya kukabiliana na swala sugu la mihadarati nchini.

4. "Umeletwa hapa na wasamaria wema." Sauti ya kike ikanieleza. Nikavuta kumbukizi…

MTIHANI WA ISHIRINI NA TATU

1. Lazima

   Wewe umemaliza chuo kikuu miaka minne iliyopita. Andika barua ya kuomba kazi ya ualimu na uiambatanishe na wasifu kazi.

2. Usalama umekuwa changamoto nchini kwa muda sasa. Pendekeza hatua ambazo serikali yafaa kuchukua ili kuimarisha usalama.

3. Mstahimilivu hula mbivu

4. Andika insha itakayomalizika kwa maneno haya…. Niliyakumbuka maneno ya mwalimu mkuu, machozi yalitoka njia mbilimbili. Hayawi hayawi huwa.

MWALIMU ONYANGO. DIRA SERIES #10. 0707311302. DIRA YA INSHA. HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA. ©2021

MTIHANI WA ISHIRINI NA NNE

1. Usalama kijijini mwenu umezorota sana siku hizi. Wewe kama Chifu wa kata lenu mwandikie barua Mkuu wa Polisi ukilalamikia hali hii. Nakala za barua hii ziwafikie:

i) Mkuu wa Wilaya.

ii) Kamishina wa Polisi.

2. Andika kisa kudhihirisha ukweli wa methali:
   Ujana ni moshi, ukenda haurudi.

3. Mafuriko yamesababisha madhara mengi humu nchini. Jadili.

4. Andika insha itakayomalizikia kwa maneno haya: ...wanakijiji walifurahia kupatikana kwa utulivu hata ingawa taswira ya maovu yaliyofanywa haikufutika akilini mwao.

MTIHANI WA ISHIRINI NA TANO

Wewe ni katibu wa jopo lililoteuliwa kuchunguza changamoto zinazokabili uchapishaji wa vitabu vya Kiswahili nchini. Andika ripoti hiyo.

2. Samaki mkunje angali mbichi.

3. Serikali za ugatuzi zitakuwa na manufaa kwa maendeleo ya nchi.Jadili.

4. Andika insha itakayomalizika kwa maneno haya.....

   Niliyakumbuka maneno ya mwalimu mkuu,machozi yalitoka njia mbilimbili.Hayawi hayawi huwa.

MWALIMU ONYANGO. DIRA SERIES #10. 0707311302. DIRA YA INSHA. HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA. ©2021

MTIHANI WA ISHIRINI NA SITA

1. Lazima.

Kuna changamoto nyingi zinazokumba wanafunzi wanaokamilisha masomo ya kidato cha nne.

Huku ukitaja baadhi ya changamoto hizi, fafanua jinsi watakavyokabiliana nazo.

2. Jamii ya Kenya imeathiriwa na utamaduni wa kigeni kwa kiwango kikubwa. Thibitisha.

3. Baada ya dhiki faraja.

4. Andika insha utakayokamilisha kwa maneno yafuatayo.

"…Hakimu alikariri fungu la sharia kisha akaagiza nirudishwe rumande hadi ushahidi na stakabadhi muhimu ziwasilishwe kortini".

MTIHANI WA ISHIRINI NA SABA

1. Ukiwa mhariri wa gazeti moja hapa nchini, andika tahariri ukifafanua jinsi mivutano kati ya vyma vya kisiasa inavyoathiri ustawi wa taifa.
2. Nchi nyingi za Afrika zimekabiliwa na mizozo inayoelekea kuzusha vita vya wenyewe kwa wenyewe. Fafanua chanzo cha matokeo ya mizozo hii.
3. Andika kisa kinachodhihirisha ulweli wa methali kuwa "sikio la kufa halisikii dawa".
4. Andika insha itakayoanzia, "Nilikuwa nimetua katika uwanja wa ndege na kwenda kuuchukua mkoba wangu. Mara mbwa wa polisi akaanza kunifuata na kuninusanusa. Ghafla alitoa mbweko mkali uliowafanya polisi kuanza kunifuata."

MWALIMU ONYANGO. DIRA SERIES #10. 0707311302. DIRA YA INSHA. HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA. ©2021

MTIHANI WA ISHIRINI NA NANE

1. Kumekuwa na visa vya upiganaji wa kabila zinazozania mifugo katika Kaunti yako. Wewe kama gavana wa kaunti hiyo watumie waathiriwa risala ukiwaeleza hatua zinazoweza kuchukuliwa kupunguza vita hivyo.

2. Hatua ya serikali kuu kumpa kila mwanafunzi wa darasa la kwanza tarakilishi ni ya manufaa sana. Jadili.

3. Andika insha inayodhihirisha methali
   Mwenda tenzi na omo marejeo ni ngamani

4. Anza kwa
   Walipofungua mlango huo, wengi hawakuweza kuzuia hisia zao. Walitoa kwi! kwi! kwa maafa walioshuhudia…

MTIHANI WA ISHIRINI NA TISA

1. **SWALI LA LAZIMA**.
   Visa vya dhuluma dhidi ya mtoto wa kike vimeongezeka sana nchini.Andika taarifa ya hali hii nchini.

2. Uhifadhi wa mazingira una manufaa mengi kwa binadamu .Thibitisha.

3. Kutangulia si kufika.

4. Malizia kwa……tulifukumana huku nyuso zetu zikiwa na tabasamu la matumaini.

MWALIMU ONYANGO. DIRA SERIES #10. 0707311302. DIRA YA INSHA. HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA. ©2021

MTIHANI WA THELATHINI

1. Wewe ni katibu wa kamati ya maslahi ya klabu ya wasanii chipukizi mtaa wa Rehema. Andika kumbukumbu za mkutano uliofanywa hivi karibuni kujadili suala la usalama uliozorota.
2. Ufisadi umekuwa janga linalohitaji kujitolea ili kupiga vita. Jadili.
3. Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali: Ulimi huuma kuliko meno.
4. Tunga kisa kinachomalizika kwa maneno haya:
   …….hapo ndipo iliponipambazukia kuwa nilikuwa naogelea baharini pekee, kinyume na wenzangu wote.

SEHEMU YA C:

MASWALI YA KCSE 2007-2019(REJELEA MAJIBU KATIKA KARATASI ZA KCSE, MIONGOZO)

2007

1. Andika barua kwa mhariri wa gazeti ukiilalamikia hali ya watu nchini kwenu kuhamia mataifa ya nje kwa wingi.
2. Eleza vile tatizo la uhaba wa maji iinavyoweza kutatuliwa hapa nchini.

2008

1. Andika tahariri kwa gazeti **la** *Raia ukieleza* hatua zinazochukuliwa nchini ili kumwendeza kielimumtoto msichana.
2. "Ufisadi ndicho k**ikwazo kikuu** katika maendeleo ya uchumi wa **taifa** lolote." Thibitisha.

2009

1. Umealikwa kitongojini mwenu kama mgeni wa heshima katika hafla ya kuzindua kundi la wasanii wa Kikwetu. Andika hotuba utakayotoa kuonyesha umuhimu wa sanaa na michezo.
2. “Utalii una madhara mengi kuliko faida hapa nchini.” Jadili.

MWALIMU ONYANGO. DIRA SERIES #10. 0707311302. DIRA YA INSHA. HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA. ©2021

2010

1. Andika wasifu wa ndugu yako ambaye amepanga hafla ya kuchangisha pesa za kumgharamia masomo ya Chuo Kikuu.
2. Eleza hatua zinazochukuliwa na serikali kuparabana na ufisadi hapa nchini.

2011

1. Wewe kama mwanafunzi umepata nafasi ya kumhoji Mkurugenzi wa Habari nchini kuhusu umuhimu wa magazeti kwa wanafunzi washule za sekondari. Andika mahojiano hayo.
2. "Magari ya matatu yameleta faida nyingi Kapa nchini kuliko hasara." Jadili.

2012

1. Wewe ni mkuu wa Baraza la Wanafunzi shuleni mwenu. Kumekuwa na visa vyawanafunzi kukiuka sheria za shule. Andika kumbukumbu za mkutano wa baraza hili uliofanyikakujadili suala hili.
2. Andika insha kuhusu umuhimu wa vijana katika kuimarisha mshikamano wa kitaifa.

2013

1. Wewe ni meneja katika kampuni ya Jitihada ambapo pamekuwa na visa vya ukiukaji wa maadili ya kikazi. Waandikie wafanyakazi memo kuwaonya dhidi ya jambo hili.
2. "Rununu (simutamba) imeleta athari mbaya katika jamii." Jadili.

2014

1. Andika hotuba utakayowatolea wazazi, walimu na wanafunzi kuhusu umuhirnu wa ushauri-nasaha katika shule za sekondari.
2. Andika insha kuhusu jinsi raia wanavyoendeleza matumizi mabaya ya ardhi nchini.

2015

1. Wewe ni katibu wa jopokazi lililoteuliwa kuchunguza vyanzo vya ongezeko la visa vya wanafunzi katika eneo la Tekeleza kuacha shule kabla ya kukamilisha masomo yao. Andika ripoti ya uchunguzi huo.
2. Andika insha kuhusu umuhimu wa tamasha za muziki katika maisha ya vijana.

MWALIMU ONYANGO. DIRA SERIES #10. 0707311302. DIRA YA INSHA. HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA. ©2021

2016

1. Wewe ni katibu wa kamati inayochunguza jinsi ya kupambana na tatizo sugu la dawa za kulevya. Andika ripoti ukitoa mapendekezo ya kamati.
2. "Utalii una faida nyingi kuliko madhara nchini Kenya." Jadili.

2017

1. Shirika la kigeni la Tugawane limeanzisha kiwanda cha kutengeneza matofali katika eneo bunge lenu. Mwandikie mhariri wa gazeti la Mzalendo ukitoa maoni yako kuhusu faida na changamoto zinazoweza kutokana na mradi huu.
2. Andika insha kuhusu umuhimu wa vyama mbalimbali shuleni.

2018

1. Wewe ni katibu wa chama cha Walinda Mazingira Wasio na Mipaka shuleni mwenu. Andika kumbukumbu za mkutano uliofanyika kujadili suala la uharibifu wa mazingira katika eneo lenu.
2. "Udanganyifu katika mitihani haumwathiri mwanafunzi tu, bali pia jamii yake." Fafanua.

2019

1. Wewe ni mkuu wa Elimu katika kaunti ndogo ya Tuangaze. Andika hotuba utakayowatolea Maafisa wa Elimu na Walimu kuhusu umuhimu wa kustawisha vyuo vinavyotoa mafunzo ya kiufundi katika eneo lao.
2. "Usalama wa mwanafunzi unamtegemea yeye." Jadili.

SEHEMU YA D: MAELEZO MAFUPI

MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA UANDISHI WA INSHA

1. Muundo
2. Kichwa
3. Utangulizi
4. Mwili
5. Hitimisho
6. Urefu
7. Lugha
8. Hati
9. Maudhui

MWALIMU ONYANGO. DIRA SERIES #10. 0707311302. DIRA YA INSHA. HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA. ©2021

10. Uhalisia
11. Msamiati
12. Nafsi
13. Wakati
14. Muda
15. Lugha
16. Ubunifu

Aina za insha

1. Kiuamilifu
2. Mjadala
3. Methali
4. Mdokezo

Barua za kirafiki
Barua rasmi
Barua kwa mhariri
Barua pepe
Barua ya mapendekezo
Barua ya mwaliko
Risala
Hotuba
Memo
Ripoti
Kumbukumbu
Mazungumzo
Dayolojia
Mahojiano
Wasifu
Tawasifu
Wasifukazi
Tahariri
Tahakiki
Ratiba
Shajara
Tahadhari
Resipe
Taarifa
Matangazo

MWALIMU ONYANGO. DIRA SERIES #10. 0707311302. DIRA YA INSHA. HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA. ©2021

Insha za mjadala
Methali
Mdokezo

INSHA ZA MJADALA: MUKHTASARI

- Hili ni swali la pili katika 102/1
- Hizi ni insha zinazomhitaji mwanafunzi kujadili/kueleza/kufafanua jambo fulani.
- Insha hizi huhusu masuala tambuzi katika jamii.
- Insha hizi ni za aina mbili; za kufafanua/kueleza na kujadili
- Aghalabu za kufafanua humuhitaji mwanafunzi kueleza jambo fulani bila kuzingatia pande mbili.
- Za kujadili humhitaji mtahini kueleza pande mbili.
- Muhimu katika insha hizi ni kuzingatia maudhui.
- Mtahiniwa afafanue hoja saba au zaidi.
- Kila aya ianze kwa hoja na ufafanuzi ufuate.
- Aandike aghalabu kurasa mbili za A4.
- Azingatie mambo yote yaliyotajwa hapo juu katikaa uandishi wake.
- Utangulizi na hitimisho ni muhimu katika insha hizi.
- Msimamo utolewe katika hitimisho.
- Mtahiniwa azingatie wakati ulio katika swali vinginevyo atapata bakshishi.

MASWALA TAMBUZI/IBUKA

1. Ufisadi serikalini
2. Ulanguzi wa dawa za kulevya
3. Utalii
4. Ulanguzi wa binadamu
5. Teknolojia ya habari na mawasiliano [TEKNOHAMA]
6. Mitandao ya kijamii
7. Mimba za mapema miongoni mwa wanafunzi
8. Kuporomoka kwa majengo mijini
9. Unyanyapaa unaoshirikishwa na ukimwi
10. Kuchomwa kwa shule
11. Migomo ya wafanyakazi; walimu,madaktari, wahadhiri
12. Baadhi ya shule za kitaifa za bweni kufanywa shule za kutwa
13. Michezo

MWALIMU ONYANGO. DIRA SERIES #10. 0707311302. DIRA YA INSHA. HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA. ©2021

14. Matatizo yanayowakumba vijana
15. Kupigwa marufuku kwa adhabu kwa njia ya viboko katika shule
16. Utelekezaji wa watoto
17. Mizozo ya kifamilia
18. Ukabila
19. Machafuko ya kisiasa
20. Ugatuzi nchini Kenya
21. Ugaidi unaoendelezwa na Al-shabaab
22. Kuhamishwa kwa walimu wakuu
23. Kupunguzwa kwa alama za kuingia chuoni
24. Wizi wa mitihani
25. Biashara haramu
26. Kupigwa marufuku kwa ukataji wa miti
27. Mafuriko
28. Kiangazi
29. Tohara kwa watoto wa kike
30. Ajali za barabarani
31. Wanafunzi kufeli mitihani ya kitaifa
32. Wafugaji kunyang'anywa mifugo nchini Tanzania
33. Wananchi kuyachukuwa maisha yao/kujitia kitanzi
34. Swala la ardhi
35. Ulemavu
36. Waajiriwa kujiuzulu kazini
37. Uchafuzi wa mazingira
38. Mtindo mpya wa kuwasajili wanafunzi
39. Utovu wa maadili

MASWALI

1. Fafanua matatizo mbalimbali yanayowakumba vijana.
2. Eleza hatua zinazochukuliwa na serikali kuimarisha hali ya mtoto wa kike nchini Kenya.
3. Tathmini jinsi ufisadi unavyolemaza maendeleo nchini.
4. Utovu wa maadili miongoni mwa vijana husababishwa na wazazi. Jadili.
5. Eleza njia anuwai za kuhifadhi mazingira.
6. Mitandao ya kijamii ina madhara mengi kwa vijana. Jadili.
7. Fafanua njia kadha za kuepuka madhara ya mafuriko.
8. Ugatuzi ni baraka na laana nchini Kenya. Jadili.
9. Eleza njia za kuboresha elimu shuleni.
10. Fafanua mambo yanayowafanya wanafunzi kufeli mitihani ya kitaifa.
11. Vijana wana jukumu kubwa katika kuimarisha mshikamano wa kitaifa. Jadili.

MWALIMU ONYANGO. DIRA SERIES #10. 0707311302. DIRA YA INSHA. HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA. ©2021

12. Tatizo la njaa ni mwiba wa kujidunga. Jadili.
13. Fafanua umuhimu wa wananchi kushiriki katika uchaguzi nchini.
14. Eleza sababu za vijana kujiunga na makundi ya kihalifu.
15. Ni jukumu la kila mwananchi kuimarisha uchumi wa nchi. Eleza.
16. Eleza jukumu la taasisi za elimu katika kuimarisha mshikamano wa kitaifa.
17. Serikali ina jukumu la kuendeleza lugha za kiasili. Fafanua.
18. Fafanua njia mbalimbali za kuhifadhi maji.
19. Tathmini umuhimu wa misitu.
20. Uchukuzi kwa njia ya matatu una faida nyingi kuliko hasara.
21. Fafanua njia za kuimarisha amani na utulivu shuleni.
22. Rukono zina manufaa mengi kuliko madhara.
23. Eleza hatua zinazochukuliwa na serikali kukomesha ugaidi nchini.
24. Serikali inafaa kupongezwa kwa kupiga marufuku matumizi ya karatasi za kufungia bidhaa.
25. Kuongeza idadi ya vyuo vikuu nchini Kenya kumeathiri vibaya viwango vya elimu. Jadili.
26. Eleza umuhimu wa michezo mbalimbali katika maisha ya mwanafunzi.
27. Serikali yafaa kupiga marufuku ukataji ovyo wa miti.
28. Eleza njia mbalimbali za kusuluhisha migogoro ya ardhi nchini.
29. Fafanua umuhimu wa magazeti nchini.
30. Ajali za barabarani zinaweza kukomeshwa. Eleza.
31. Eleza njia za kukuza vipaji vya wanafunzi shuleni.
32. Fafanua majukumu ya tume za kikatiba nchini Kenya.
33. Eleza hatua zinazofaa kuchukuliwa na serikali kuleta utangamano miongoni mwa wananchi.
34. Miziki husababisha kudorora kwa maadili miongoni mwa vijana. Jadili.
35. Eleza sababu za ongezeko la vijana wa kurandaranda mitaani.

- WAZOESHE WANAFUNZI WAKO KUANDIKA INSHA ZA KURASA MBILI ZA A4. ANGALAU INSHA MOJA KWA KILA JUMA.
- WANAFUNZI WASOME INSHA ZA WENZAO DARASANI NA KUKOSOANA.
- ZILE ZILIZO BORA ZISOMWE DARASANI.
- MAKOSA YA SARUFI NA HIJAI YAANIKWE.
- SWALA LA HOJA KATIKA INSHA LIZINGATIWE MNO.

MWALIMU ONYANGO. DIRA SERIES #10. 0707311302. DIRA YA INSHA. HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA. ©2021